

**WIND**  
**ARE YOU IN?**

**HATI YA  
KUTANGAZA  
SERA YA  
BARAZA LA  
KIMATAIFA LA  
NISHATI YA  
UPEPO YA  
MKUTANO WA  
COP27**



**#WINDAREYOUIN**  
**WWW.WINDAREYOUIN.COM**



## Hati ya Kutangaza Sera ya Baraza la Kimataifa la Nishati ya Upepo ya Mkutano wa COP27 | 2022

Ulimwengu uko katika nyakati hatari, ambapo unakabiliwa na changamoto za kipekee za usalama wa nishati, mfumuko wa bei unaozidi kuongezeka na kupungua kwa kipindi cha muda wa kudhibiti hali hatari ya ongezeko la joto duniani. Mkutano wa COP27 mnamo mwezi wa Novemba 2022 unatoa fursa ya kipekee kwa serikali za nchi duniani kote kuchukua hatua thabiti kuhusu mabadiliko ya hali ya anga, kuboresha usalama wa nishati na kutoa ahadi dhahiri na zinazoweza kutekelezwa za kuunda mfumo safi, salama na wa bei nafuu wa nishati unaotokana na nishati inayoweza kutumika tena.

Sekta ya uzalishaji wa nishati ya upepo iko tayari kushirikiana na serikali za nchi, biashara, jamii na raia ili kufikia viwango vipya vya ukuaji wa nishati ya upepo na mabadiliko ya kweli ya mfumo.

**Je, utashiriki?**

Mgogoro wa sasa wa kimataifa wa nishati na mzozo ulioko nchini Ukreni umefichua uhalisia dhahiri na gharama za kutegemea kwa muda mrefu nishati inayotokana na visukuku isiyothabiti. Tusipoharakisha juhudi za kuchukua hatua ya kuongeza kiwango cha uzalishaji wa nishati ya upepo na nishati inayoweza kutumika tena katika muongo huu, tutakosa kutimiza lengo letu la kimataifa la kukomesha kabisa uchafuzi wa anga kufikia mwaka wa 2050 – na tutakuwa katika hatari ya kukabiliwa na vitisho vya ustaarabu vya mzozo wa kijamii, uharibifu wa mazingira usioweza kurekebisha na matatizo ya kiuchumi.

Mikakati ya [kukomesha kabisa uchafuzi wa anga](#) na [makubaliano ya kisayansi](#) ni dhahiri kabisa: Hatua za kukomesha haraka matumizi ya nishati inayotokana na visukuku na kuharakisha juhudi za uzalishaji wa nishati inayoweza kutumika tena zinahitaji kuchukuliwa haraka iwezekanavyo ili kufanikisha hatua ya kupunguza



zaidi uchafuzi wa anga katika sekta zote za uchumi, na kudumisha lengo la kupunguza kiwango cha joto duniani kwa kiwango cha 1.5°C. Shirika la IPCC limetaka shughuli za kimataifa za uzalishaji wa nishati ya kaboni kufikia kiwango cha juu zaidi kabla ya mwaka wa 2025 na kupungua hadi nusu kufikia mwaka wa 2030 – na linaamini kuwa hili linawezekana kwa kukuza nia njema ya kisiasa na utekelezaji.

**Tuna zana, teknolojia na maarifa.** Sekta ina maarifa ya miongo mingi katika kujenga mifumo ya kiwango cha GW, vituo fanisi vya viwanda vya nishati safi na jopokazi la kimataifa lenye zaidi ya watu milioni 1.25. Nishati ya upepo imesababisha kupungua kwa gharama kwa kiwango kikubwa katika muongo uliopita – nishati ya pepo za bara ni mojawapo ya mifumo ya gharama nafuu zaidi ya uzalishaji mpya wa nishati katika nchi nyingi ambayo inafikia thuluthi mbili ya idadi ya watu duniani, na nishati ya pepo za baharini inazidi kuendelea kushinda nishati inayotokana na visukuku.

**Nishati ya upepo ni mojawapo ya teknolojia za gharama nafuu, thabiti na zinazoweza kutumika haraka tulizo nazo kwa sasa,** na ina jukumu la msingi katika kudumisha utoaji wa nishati, kuboresha usalama wa nishati wa kimataifa, kuhakikisha hali ya kutegemewa kwa nishati na kutimiza malengo ya upunguzaji wa viwango vya uchafuzi wa anga. Lakini ili sekta ya uzalishaji wa nishati ya upepo inawiri, inahitaji viwango vikubwa, thabiti na vinavyoonekana vya uzalishaji na mkondo mkubwa wa usambazaji wa kimataifa. Mikakati ya kufanikisha malengo ya kukomesha kabisa uchafuzi wa anga tayari inaonyesha kuwa viwango vya uzalishaji wa nishati ya upepo lazima vizidi mara nne ya viwango vya sasa kufikia mwaka wa 2030 ili kuwa katika mkondo wa kutimiza malengo yetu ya Mkataba wa Paris (angalia Kiambatisho). Kufikia mwaka wa 2050, sekta ya nishati ya upepo lazima izalishe zaidi ya thuluthi moja ya umeme wa kimataifa, kutoka 6% ya kiwango cha sasa.

Ulimwengu uko katika njia panda: Miaka kadhaa ijayo ya kufanya maamuzi itabaini iwapo tunaweza kudumisha mustakabali wa maisha ya baadaye kwa ajili ya kila mtu na mabadiliko ya nishati ya haki na usawa. Hii itahitaji uundaji wa sera dhahiri na umoja wa kimataifa ili kuhakikisha kuwa viwango vya uzalishaji wa nishati inayoweza kutumika tena vinaongezeka kwa njia thabiti, na kusambaza manufaa ya mabadiliko hayo kwa kila mtu duniani kote.

Itahitaji sekta ya nishati ya upepo kushirikiana kwa ukaribu na jamii za eneo, wadau wa jamii na sekta zingine, ili kuhakikisha kuwa sekta ya uzalishaji wa nishati ya upepo inapanuka bila kuathiri mazingira asili, raia na uchumi kwa ujumla. Na mabadiliko ya mfumo yatawezekana tu kwa matumizi ya umeme kwa kiwango kikubwa, kuimarika kwa ufanisi wa nishati na uuzaji wa nishati safi kama vile gesi ya haidrojeni inayoweza kutumika tena ili kukomesha matumizi ya nishati ya kaboni katika sekta ambazo ni vigumu kukoma kuitumia.

Kama makampuni na mashirika yanayowakilisha zaidi ya 80% ya mitambo ya upepo na minyororo ya usambazaji duniani kote, [tunazitaka serikali za nchi ziahidi kuchukua hatua za haraka ili kupunguza mabadiliko ya hali ya anga na mgogoro wa usalama wa nishati katika mkutano wa COP27 mwaka huu](#). Waundaji wa sera za kitaifa katika kila eneo la dunia lazima:



# 1

**Waongeze kiwango cha nia na viwango vya juu vya uzalishaji wa nishati ya upepo, na kuonyesha hili katika Michango Iliyobainishwa Kitaifa iliyosasishwa (NDCs, Nationally Determined Contributions) kufikia mwisho wa mwaka wa 2022, mikakati ya kina ya kitaifa ya kushughulikia mabadiliko ya hali ya anga na kukomesha kabisa uchafuzi wa anga na mipango ya muda na ya kudumu ya nishati.**

Lengo bora la muda mfupi na la kudumu katika uzalishaji wa nishati ya upepo linahitajika, kulingana na lengo la kukomesha kabisa uchafuzi wa anga na umuhimu wa usalama wa nishati. Ingawa maeneo tofauti duniani yatabadilika kwa kasi tofauti, matumizi thabiti ya nishati inayoweza kutumiwa tena au malengo ya uzalishaji yanapaswa kuwa na lengo la kufikia mwaka wa 2030, 2040 na zaidi. Kisha, hatua dhahiri za muda mfupi kwa miaka kadhaa ijayo zinahitajika ili kubadilisha malengo haya kuwa mfumo ulio tayari kutumika na ishara fanisi za uwekezaji. Malengo yanapaswa kulingana kati ya mashirika ya umma yanayosimamia hali ya anga, nishati, uchumi, mazingira, miundo msingi na wafanyakazi, ili kuhakikisha kuwa mashirika mbalimbali ya serikali yanametayarishwa ipasavyo kuyatekeleza. Malengo pia yanapaswa kujumuishwa katika mikakati ya kitaifa ya hali ya anga, mikakati ya nishati na ukuaji wa viwanda ambayo inatambua uhusiano kati ya nishati inayoweza kutumika tena ya kiwango cha mtandao, usalama wa nishati, unafuu wa gharama ya nishati, ukuaji wa kudumu, manufaa ya jamii na uchumi na kasi inayofaa ya ukuaji. Serikali za mitaa na kitaifa zinaweza pia kuzingatia mikakati ya kuhifadhi nishati ya ziada (Power-to-X) na nishati safi ya haidrojeni inayosaidiwa na viwango vikubwa vya nishati inayoweza kutumika tena ili kukomesha matumizi ya nishati ya kaboni katika sekta ambazo ni vigumu kukoma kuitumia kama vile viwanda vya uzalishaji wa bidhaa nyingi na nzito, utengenezaji wa ndege na vyombo vya majini, au ili kuwezesha sekta ya kilimo isiyoathiri mazingira.




# 2

**Kuboresha mipango ya utoaji wa vibali haraka iwezekanavyo kwa miradi ya uzalishaji wa nishati inayoweza kutumika tena ya kiwango cha mtandao ili kuongeza kasi ya uzalishaji wa nishati ya upepo na kujenga mfumo wa mradi unaolingana na malengo ya kukomesha kabisa uchafuzi wa anga katika sekta ya nishati.**

Kuongeza viwango vya uzalishaji wa nishati ya upepo ni ushindi kwa pande zote kuhusiana na upunguzaji wa bei za nishati, kuchochea uwekezaji, ukuaji wa uchumi na uundaji wa nafasi za kazi na kutimiza malengo ya hali ya anga huku ukiendeleza usalama wa nishati. Lakini mipango migumu kwa ujumla ya utoaji wa vibali inapunguza kasi ya uzalishaji katika baadhi ya masoko maarufu zaidi duniani ya nishati ya upepo, kutoka Italia hadi India. Katika nchi zingine, karibu muongo mmoja wa muda wa ujenzi na ukamilishaji wa mradi unahitajika ili kubuni mradi wa uzalishaji wa nishati ya upepo. Hii ni changamoto ya kimataifa ambayo ni lazima ishughulikiwe kwa kiwango kikubwa ili kuongeza kasi ya uzalishaji wa nishati inayoweza kutumika tena. Changamoto ya janga la COVID-19 imeonyesha kuwa muundo msingi mkubwa wa dijitali na halisi unaweza kuletwa pamoja wakati wa dharura ili kupanga upya taratibu za usimamizi na mikondo ya usambazaji kulingana na maslahi ya kitaifa. Licha ya suala la usalama wa nishati na mgogoro wa hali ya anga, kasi hii inapaswa kutumika katika miradi ya uzalishaji wa nishati inayoweza kutumika tena na muundo msingi wa ufanikishaji.

**Utoaji wa vibali ulioboreshwa unaweza kufanikishwa huku ukiendeleza mwingiliano bora wa sekta na watumiaji wengine wa ardhi/bahari na jamii za eneo, pamoja na kutii viwango vya juu vya mazingira na jamii. Kwa uongozi thabiti, malengo ya juu ya uzalishaji wa nishati inayoweza kutumika tena na mpango dhahiri wa utoaji wa vibali zinaweza kuleta usawa wa maslahi kati ya wadau wengi. Hatua zifuatazo zinapaswa kuzingatiwa, kati ya nyinginezo:**




## Hati ya Kutangaza Sera ya Baraza la Kimataifa la Nishati ya Upepo ya Mkutano wa COP27 | 2022

- Kikomo cha vipindi vya muda ulioamrisha wa kuanzishwa na kukamilishwa kwa shughuli ya utoaji wa vibali kwa viwanda vya uzalishaji wa nishati inayoweza kutumika tena, kama vile ahadi ya hivi karibuni kutoka kwa Baraza la Nishati la Ulaya (EU Energy Council) ili kuongeza kasi ya uzalishaji wa nishati inayoweza kutumika tena ya eneo ili kuzingatia “maslahi ya jumla ya umma,” na muda wa mwisho wa miaka 2 ya kutoa vibali kwa miradi;
- Mamlaka za jumla na mashirika ya kujitegemea kushirikiana na wabunifu kuhusu uboreshaji wa shughuli za utambuaji wa eneo na utoaji wa vibali, kama vile mchakato wa “kutoa huduma zote katika sehemu moja”;
- Hifadhidata za dijitali na zinazoweza kufanyiwa utafutaji za usajili wa ardhi, amri za mamlaka ya eneo na rekodi za upinzani wa eneo kwa mradi, ambazo zinaweza kuharakisha ubainishaji wa maeneo ya mradi;
- Mwongozo unaolingana wa matumizi ya ardhi na bahari katika kiwango cha kitaifa na eneo, unaotoa kipaumbele kwa miradi inayoendeleza usalama wa nishati na kanuni za “Usisababishe Madhara Makubwa”;

## **Hati ya Kutangaza Sera ya Baraza la Kimataifa la Nishati ya Upepo ya Mkutano wa COP27 | 2022**

- **Mbinu za dharura za kuendeleza na kuwezesha ushirikiano wa kiufundi na kisayansi kwa mizozo ya kisheria ili kuzuia vipindi virefu vya ucheleweshaji wa miradi muhimu ya miundo msingi;**
- **Mbinu ya kimkakati ya kudhibiti athari kwa bioanuai na urejeshaji wa mazingira ya asili, ambayo inatambua jukumu la nishati ya upepo katika upunguzaji wa athari mbaya zinazotokana na mabadiliko ya hali ya anga;**
- **Taratibu zinazoingiliana za utoaji vibali kwa viwanda vya uzalishaji wa nishati ya upepo wa baharini (ambavyo vina vipindi virefu vya utengenezaji), kama vile kuruhusu utekelezaji wa wakati mmoja wa utathmini wa mazingira na ufikiaji wa mtandao, na kuhakikisha muda wa kutosha wa ujenzi ili muda wa vibali vilivyotolewa usiishe mapema; na**
- **Uchunguzi wa haraka wa mamlaka za usimamizi ili kuwezesha kufunguliwa upya kwa viwanda vilivyopo vya uzalishaji wa nishati ya upepo wa bara ambavyo muda wa matumizi ya tabo unakaribia kuisha, kushughulikia taratibu za EIA, upanuzi wa eneo la usambazaji na utoaji wa leseni ya kituo.**





# 3

## **Kuahidi kuweka mipango ya hatua za kujenga haraka mitandao ya ujumuishaji wa nishati safi na ukomeshaji wa matumizi ya nishati ya kaboni katika sekta zote.**

Chini ya thuluthi moja ya uwekezaji wa umma na wa kibinafsi wa nishati kwa sasa unalenga suhulu za mtandao na za uhifadhi. Raslimali zilizotengwa kwa mpango, ujenzi na kuboresha mitandao kwa ajili ya mfumo wa nishati wa siku zijazo lazima ziongezwe kwa kiwango cha juu ndani ya muongo huu. Ujenzi wa mitandao salama, mahiri na inayobadilika kwa urahisi lazima ulingane na kasi ya migawo mikubwa ya nishati inayoweza kutumika tena kwenye mfumo. Hii itahitaji ushirikiano kati ya wasimamizi wa mfumo, wadhibiti, huduma za matumizi na sekta ili kutekeleza mpango wa kudumu wa uendelezaji kuhusu upanuzi wa mtandao na uimarishaji, kutumia umeme katika sekta ya usafiri na sekta zingine, kuunda masoko ya eneo kwa uuzaji wa nishati nje ya nchi na biashara na kuhakikisha usalama wa mtandaoni.

Mpango na usimamizi wa mtandao unapaswa kuruhusu miundo bunifu ya ujenzi, ikijumuisha “vituo” vingi vya nishati ya upepo vilivyonganishwa na “visiwa vya nishati” ya upepo wa baharini vilivyonganishwa kwa masoko kadhaa au maeneo ya bei. Mpango wa mtandao na mbinu za soko kama vile minada zinapaswa pia kuchangia katika suluhu za kuhifadhi, kama vile maji yanayopigwa kwa pampu, betri za kiwango cha huduma za matumizi na vifaa vikubwa vya kuhifadhi nishati ya ziada (Power-to-X), ambavyo vinaweza kupunguza msongamano wa mitandao na kusaidia usawazishaji. Hatua zinazoweza kuchukuliwa kwa muda mfupi zinajumuisha kukagua vipindi vya muda wa kufanya maamuzi ya muunganisho wa mtandao na kuhakikisha mifumo ya kudumu, thabiti na inayowezesha uwekezaji ya mtandao na huduma zinazobadilika kwa urahisi imewekwa ili kuruhusu uwekezaji wa kutosha na unaotarajiwa kutoka kwa sekta ya umma na ya kibinafsi na mashirika mbalimbali. Miundo mingine ya biashara inaweza kupunguza zaidi msongamano wa mitandao, kama vile watumiaji kushiriki eneo la huduma ya nishati inayoweza kutumika tena.

# 4

## Kukuza masoko ya nishati ya siku zijazo.

Katika nchi nyingi, masoko ya umeme hutatizika kutuma ishara muhimu na kwa muda unaofaa za uwekezaji zinazolingana na malengo ya kukomesha kabisa uchafuzi wa anga. Baada ya mgogoro wa sasa wa nishati kutatuliwa, athari ya orodha ya ustahiki katika masoko huru zaidi itamaanisha kuwa mapato ya soko la jumla ya nishati inayoweza kutumika tena hufifia wakati usambazaji wa nishati ya upepo na sola unapoongozeka. Shinikizo hili la bei litaongezeka tu kwa viwango vidogo vinavyopatikana vya uzalishaji wa nishati, hali ambayo huongeza viwango vya riba na ongezeko la mahitaji kwa bidhaa zinazohusiana na mabadiliko na madini muhimu. Katika nchi zingine, muundo wa kupiga mnada umehimiza “utoaji wa zabuni mbaya,” ambao kimahususi haujakuwa na manufaa na unadunisha uwezo wa kujitegemea wa mkondo wa usambazaji wa nishati inayoweza kutumika tena ili kuchukua nafasi ya nishati inayotokana na visukuku.

Masoko ya nishati lazima yabadilike ili kuchochea uwekezaji katika uzalishaji wa nishati inayoweza kutumika tena na muundo msingi wa nishati, ikiwa tunataka kubadili na kutumia mfumo wa nishati wa siku zijazo ambao unaweza kubadilika kwa urahisi, unaoshughulikia mahitaji, unaotegemewa na unaotegemea mgawo mkubwa (ikiwa si 100%) wa nishati inayoweza kutumika tena. Ukandarasi wa ununuzi unapaswa kuendelezwa na mbinu rahisi na ya wazi ya bei ambayo inaimarisha mapato na kushiriki hatari kati ya watumiaji na wazalishaji. Katika nchi zingine, hii inahitaji kukagua mipango ya kupiga mnada ili kuhakikisha vipindi thabiti, endelevu na vilivyopangwa na mikataba mingi ambayo inaweza kuchochea hali ya kibiashara ya uwekezaji kwa mkondo wa usambazaji, na kubadilisha ununuzi kutoka msingi wa “gharama ya chini” hadi mbinu ya “thamani ya juu ya pesa”.





# 5

## **Kuepuka utegemeaji wa muda mrefu wa uzalishaji wa nishati inayotokana na visukuku katika mgogoro wa sasa wa usalama wa nishati.**

Serikali za nchi duniani kote zinakabiliwa na maamuzi magumu katika usawazishaji wa mahitaji ya usalama wa nishati wakati wa bei zinazobadilika za nishati inayotokana na visukuku na malengo ya hali ya anga. Lakini waundaji wa sera lazima wawe na udhahiri katika uundaji wa sera na mikakati yao ya ushughulikiaji: Kasi ya ujenzi wa miradi mipya ya nishati inayoweza kutumika tena ya kiwango cha mtandao inapaswa kutambuliwa na kupewa kipaumbele kuliko uwekezaji katika muundo msingi wa nishati inayotokana na visukuku panapowezekana. Nishati ya upepo iko tayari kuchukua nafasi ya uzalishaji wa nishati inayotokana na visukuku katika nchi mbalimbali duniani kote, ambayo inatoa nishati ya bei nafuu, inayoweza kuongezwa zaidi na isiyo na gesi ya kaboni kabisa katika vigezo vya kiwango kikubwa. Mtindo huu unapaswa kuharakishwa katika mgogoro wa sasa; masuala yoyote ya muda mfupi ya usalama wa nishati lazima yashughulikiwe ili kuepuka kupunguza kasi ya upanuzi wa miradi ya uzalishaji wa nishati inayoweza kutumika tena au kuunda mali za kukwama kwa kipindi kirefu. Serikali na mashirika ya fedha yanapaswa kutobadilisha ahadi zake za kuondoa matumizi ya nishati inayotokana na visukuku na kuondoa ruzuku za gharama ya juu/chini ya nishati inayotokana na visukuku, huku yakiongeza kwa kasi uzalishaji wa nishati safi. Kuharakisha ufanisi wa nishati na juhudi za kutunza nishati kwa kipindi cha muda mfupi kunaweza pia kupunguza mgogoro wa sasa wa nishati.

# 6

## Kubuni sera thabiti na za jumla za kuwezesha mabadiliko ya nishati ya haki na usawa.

Mabadiliko ya nishati yanayotii lengo la upunguzaji wa kiwango cha joto duniani kwa kiwango cha 1.5°C yanasababisha athari nzuri kwa jamii na uchumi kwa ujumla ikilinganishwa na sera za sasa, kulingana na IRENA, ikijumuisha kazi nyingi zinazoundwa kupitia uwekezaji katika miradi ya uzalishaji wa nishati inayoweza kutumika kwa kiwango kikubwa, uimarishaji wa mtandao na ufanisi wa nishati. Ushirikiano wa kimataifa kutoka Kaskazini hadi Kusini na uaminifu utakuwa muhimu katika kuhakikisha migawo ya mabadiliko ya nishati inasambazwa kwa usawa kwa kila mtu. Nishati ya upepo tayari inaendeleza maendeleo ya kudumu katika jamii mbalimbali duniani kote na inaweza kuwa na jukumu muhimu katika kuunda kazi za maana na bora, huku ikiimarisha mizunguko ya fedha ili kuwezesha ukuaji thabiti usioathiriwa na hali ya anga katika nchi zinazokua. Uoanifu thabiti wa sera za kitaifa za nishati, hali ya anga, biashara na ukuaji wa viwanda unaweza kuendeleza uundaji wa thamani ya haki na kudumu nchini kadri mabadiliko yanavyoendelea kuimarika. Kupitia mipango ya umma na ya kibinafsi ya kutoa mafunzo ya ujuzi mpya na mabadiliko ya wafanyakazi, sekta inayokua ya uzalishaji wa nishati ya upepo inatoa nafasi za kazi katika uzalishaji wa nishati safi kwa wafanyakazi waliopoteza kazi kutokana na mabadiliko ya nishati, kama wale wanaofanya kazi katika uzalishaji wa nishati inayotokana na visukuku na sekta saidizi.





# 7

## Kuhakikisha ufadhili wa kitaifa na eneo unatii viwango thabiti na unaendeleza malengo ya kupunguza kiwango cha joto duniani kwa kiwango cha 1.5°C.

Hakuna ukosefu wa ufadhili kwa uzalishaji wa nishati ya upepo mahali ambapo kuna mazingira mazuri ya uwekezaji. Lakini ili kuharakisha kwa pamoja kuinua viwango vya uzalishaji wa nishati inayoweza kutumika tena, ufadhili katika sekta ya nishati – iwe ni ufadhili wa mauzo ya nje ya nchi, ufadhili wa serikali au ufadhili wa kibinafsi – lazima ubainishwe chini ya kanuni za “Usisababishe Madhara Makubwa” ambazo zinashughulikia athari kwa jamii na mazingira, na kuepuka hatari za kuanzisha miradi ya kukwama ya uzalishaji wa nishati inayotokana na visukuku. Malengo ya hali ya anga yanapaswa kulingana katika wizara zote za fedha, benki za maendeleo na mashirika ya mikopo ya mauzo ya nje ya nchi (ECA) ili kuoanisha matumizi ya fedha za umma na nishati inayoweza kutumika tena na malengo ya ukuaji. Mashirika zaidi yanapaswa kujitolea kwa ahadi iliyotolewa na mashirika 39 katika COP26 ya kuoanisha msaada wa umma wa kimataifa katika kuwezesha mabadiliko ya nishati safi na kukomesha hali ya kutegemea matumizi ya nishati inayotokana na visukuku.

Ufadhili wa hali ya anga unapaswa kutolewa kwa kiwango cha mradi katika nchi zinazokua na Nchi za Uchumi wa Kiwango cha Chini (LDC, Least Developed Countries), pamoja na kutohatarisha vyombo na zana, kama vile kutoka kwa benki za maendeleo au ECA. Serikali pia zinapaswa kuzingatia kutoa ufadhili wa kujiimarisha tena kutokana na athari za janga la COVID katika muundo msingi wa uzalishaji wa **nishati ya upepo**. Ukuzaji wa uwezo na msaada wa kiufundi kutoka kwa mashirika mbalimbali, mashirika ya umma na wahisani unapaswa kujumuisha mitazamo ya sekta ili kuhakikisha ufanisi bora katika uimarishaji wa mifumo ya kutegemewa ya mradi wa uzalishaji wa nishati inayoweza kutumika tena.

# 8

## Kuendeleza utekelezaji wa kanuni za kimataifa kuhusu bei za nishati ya kaboni, hasa Vifungu vya 6.2 na 6.4 vya Mkataba wa Paris.

Mbinu fanisi na za kutegemewa za soko za kuweka bei ya nishati ya kaboni zinaweza kutoa ishara thabiti za soko za kuchochea uwekezaji katika teknolojia za uzalishaji wa nishati ya kiwango kidogo cha kaboni. Mkutano wa COP26 na Bonn wa 2022 ulishuhudia maendeleo ya kanuni za uhamishaji wa kimataifa wa mikopo ya uzalishaji wa nishati ya kaboni na Mbinu ya Maendeleo ya Kudumu ya biashara, lakini kazi zaidi inahitajika ili kuanza kutekeleza kanuni hizi ili kutambua kwa ufanisi gharama za kiuchumi na kijamii za uchafuzi wa anga. Desturi bora za mbinu hizi zinajumuisha kukomesha utoaji wa gesi ya kaboni katika chanzo na vipimo dhahiri na kanuni za uthibitishaji za soko la kimataifa la nishati ya kaboni.




Sisi, tuliotia saina, tunazitaka serikali na mashirika husika kutambua migogoro ya sasa ya hali ya anga na nishati, na kuchukua hatua thabiti na ya pamoja katika COP27 ili kuharakisha uzalishaji wa nishati inayoweza kutumika tena. Kabla ya shughuli ya Kuchukuliwa kwa Rekodi za Hisa za Kimataifa itakayokamilika katika mkutano wa COP28 mwaka ujao, tayari ni dhahiri kuwa kuna fursa nzuri zaidi, uwezekano na haja ya kuharakisha uzalishaji wa nishati ya upepo duniani kote. Hii ni muhimu si tu kwa ajili ya kukomesha uzalishaji wa nishati ya kaboni katika mifumo ya nishati, lakini kuboresha upatikanaji wa nishati katika nchi zinazokua bila kutegemea zaidi uwekezaji katika uzalishaji wa nishati ya mafuta kwa muda mrefu.

Sekta ya kimataifa ya uzalishaji wa nishati ya upepo iko tayari kutoa msaada wetu kamili kwa serikali za nchi, mashirika ya umma na mashirika yasiyo ya serikali kwa pamoja ili kudumisha jukumu la msingi la nishati ya upepo katika mfumo safi na thabiti wa nishati, na kuleta mabadiliko ya nishati ya haki na usawa kwa wote.

**Tarehe 22 Septemba 2022**  
**Orodha ya waliotia saina:**




# Hati ya Kutangaza Sera ya Baraza la Kimataifa la Nishati ya Upepo ya Mkutano wa COP27 | 2022





Annex

Annual global wind installations must quadruple by 2030 to get on-track for net zero



Source: GWEC Market Intelligence; IEA Net Zero by 2050 Roadmap (2021). Projected new wind capacity from 2026-2030 assumes a ~6.6-7.0% CAGR, based on GWEC's projected CAGR from 2021-2026. It also accounts for ~34 GW in global decommissioned capacity from 2026-2030 based on 25-year turbine lifetime. Capacity gap figures are estimations based on the IEA Roadmap milestone for 2030. Cumulative global installations for wind energy are roughly in alignment with the IRENA World Energy Transitions Outlook: 1.5°C Pathway (2021). This data represents new capacity, cumulative capacity and decommissioned capacity, and does not include an estimate of repowering installations to replace the ~34 GW in decommissioned turbines globally.